**HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI MAHMOUD THABIT KOMBO (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA SERA YA MAMBO YA NJE YA MWAKA 2001 – TOLEO LA 2024**

**TAREHE 19 MEI, 2025 DAR ES SALAAM**

***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwana Diplomasia wetu Namba Moja;***

***Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;***

***Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu Viongozi, Mwenyekiti na Wajumbe wa NUU;***

***Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa hapa nchini;***

***Wageni wote waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Kazi Iendelee!***

***Habari za Mchana.***

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutukutanisha hivi leo.

Pili, kwa unyeyekevu na heshima kubwa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amiri Jeshi Mkuu na Mwanadiplomasia wetu Namba Moja, kwa kuridhia kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii adhimu ya uzinduzi wa *Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 – Toleo la Mwaka 2024*.

***Mheshimiwa Rais***

Kipekee nakushukuru kwa kuendelea kuniamini mimi na viongozi wenzangu, kukusaidia kutekeleza majukumu ya kusimamia uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine, Jumuiya za kikanda na Mashirika ya Kimataifa. Kwa niaba ya viongozi wenzangu na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naahidi kwamba tutaendelea kutekeleza vyema majukumu uliyotupa na unayoendelea kutupatia kwa weledi, uzalendo, bidii na maarifa makubwa, kwa maslahi ya taifa letu.

Kwetu sisi tunaona fahari kufanya kazi nawe Mheshimiwa Rais kwa kuwa umekuwa kiongozi unayetekeleza kwa vitendo yale unayosema na kuahidi. Hakika umekuwa chachu na nguzo muhimu ya kuimarisha diplomasia yetu kupitia ziara za kiserikali na kikazi, kushiriki katika mikutano, kufanya majadiliano na wabia wa maendeleo au kuitangaza Tanzania kimataifa. Hilo linathibitisha azma yako ya kukuza uhusiano wa uwili, kikanda na kimataifa, kama ambavyo uliieleza bayana wakati ukilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2021 jijini Dodoma.

Niseme tu kuwa, unatupa ari ya kujituma zaidi katika kuendelea kuunga mkono juhudi zako za kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi hii. **Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana !!**

***Mheshimiwa Rais,***

Leo ni siku mahsusi na ya kihistoria kwa diplomasia ya nchi yetu, kwakuwa tunazindua Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 - Toleo la mwaka 2024. Nitoe msisitizo kuwa, kinachozinduliwa leo siyo sera mpya bali ni sera iliyofanyiwa maboresho makubwa yatakayolisukuma mbele zaidi taifa letu kwa kuimarisha ushiriki na ushindani wetu katika siasa na maendeleo ya kimataifa. Sera ile ya mwaka 2001 ilibeba misingi, malengo na mikakati ambayo mingi itaendelea kuwa nguzo muhimu kwa nchi yetu kwa miongo ijayo. Hata hivyo, mtakubaliana nami kuwa, baada ya kipindi cha takriban miaka 24 tangu kutungwa kwa Sera hiyo, kumetokea mabadiliko mengi hapa nchini, barani Afrika na duniani. Tanzania ya leo na kesho inahitaji sera madhubuti inayozingatia mazingira mapya ya kidunia na maslahi mapana ya taifa letu.

***Mheshimiwa Rais,***

***Wageni waalikwa,***

Kwa mantiki hiyo, sambamba na uzinduzi huu, tunayo kila sababu ya kusherekea mafanikio na hatua tuliyofikia, na vilevile kujiwekea ahadi ya kupata mafanikio zaidi kama Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 zinavyotuelekeza. Ni matarajio yetu kuwa nchi yetu itakuwa ya

uchumi wa kipato cha kati cha juu ifikapo ukomo wa dira hizo. Tuna shauku ya kuwa nchi yenye mchango mkubwa katika uchumi wa dunia na sauti yenye ushawishi katika uhusiano wa kibiashara ya kimataifa. Ni matamanio yetu kama Wizara kwa Tanzania kuendelea kuwa kisiwa cha amani, utulivu, umoja na yenye mchango mkubwa katika ulinzi wa amani kwingineko duniani. Sera ya Mambo ya Nje ya 2001 (Toleo la 2024) ni nyenzo ya kimkakati kwa ajili ya kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendana na kukabiliana kikamilifu na mazingira ya kimataifa yanayobadilika na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa kwa ufanisi zaidi. Lengo kuu ni kuendelea kulinda na kutetea maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia diplomasia makini na shirikishi.

**Mchakato wa Mapitio ya Sera**

***Mheshimiwa Rais,***

Mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 yalianza mnamo mwaka 2017 kufuatia maelekezo ya viongozi wakuu na madhumuni ya kuifanya nchi yetu iendane na mabadiliko ya kiuchumi ya dunia kwa zama hizi tulizonazo. Hivyo, kabla ya kutekeleza jukumu hili, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya mwaka 2001 ili kubaini iwapo inakidhi au inapaswa kufanyiwa maboresho.

Tathmini hiyo ilibainisha kuwepo kwa mafanikio katika kufikia malengo yaliyojumuishwa kwenye Sera hiyo katika muktadha wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mathalan, tathmini ilidhihirisha kuwa Tanzania imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kulinda amani na

usalama katika ukanda unaotuzunguka, barani Afrika na duniani kupitia mchango wake wa walinda amani na jitihada za upatanishi na usuluhishi wa migogoro katika mataifa mengine.

Kadhalika, tathmini ilionesha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya kiuchumi, kiasi cha kwamba mwaka 2020 Benki ya Dunia ilitangaza kuiondoa katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha chini na kuiweka katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini. Hatua hiyo ilifikiwa kutokana na utekelezaji wa sera madhubuti za kuchochoea ukuaji wa uchumi mpana, uwezeshaji wananchi kiuchumi, uwepo wa mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji yaliyochangia katika ukuaji wa sekta binafsi.

Aidha, mafanikio hayo yalitokana na ushirikiano madhubuti baina ya Tanzania na wabia wa maendeleo, ambao wameendelea kuchangia juhudi za Serikali katika kusogeza huduma kwa wananchi na kutekeleza miradi ya kitaifa ya maendeleo.

Kwa upande wa ushirikiano wa kikanda, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika mtangamano wa kikanda kupitia uanachama wake katika jumuiya za kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambapo siyo tu imeshiriki kuimarisha mtangamano wa kiuchumi, bali pia imeshiriki katika kuimarisha ujirani mwema, ulinzi na usalama wa ukanda huu. Sanjari na hilo, Tanzania imekuwa na ushiriki mzuri katika diplomasia

ya kimataifa (*multilateral diplomacy*) kupitia Umoja wa Mataifa na mashirika yake, pamoja na majukwaa mengineyo ya kimataifa.

***Mheshimiwa Rais,***

Licha ya mafanikio niliyoainisha, tathmini ya utekelezaji wa Sera ya mwaka 2001 ilibainisha kuwepo kwa changamoto zilizofifisha kasi ya kufikia malengo ya Sera hiyo kwa ufanisi na tija zaidi. Baadhi ya changamoto hizo ni mfumo hafifu wa uratibu. Hapa niseme bayana kuwa hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na fikra potofu kuwa mtekelezaji wa Sera ni Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje pekee au baadhi ya Taasisi ndani ya Serikali; na utekelezaji hafifu wa itifaki, mikataba na makubaliano ya uwili, kikanda na kimataifa tuliyosaini.

***Mheshimiwa Rais,***

Sanjari na hilo, tathmini imeonesha uwepo wa masuala mapya yanayohitaji mwongozo wa kisera ili kuongeza ufanisi na msukumo katika utekelezaji wake. Baadhi ya masuala hayo ni utambuzi wa diaspora na mchango wao katika maendeleo ya taifa; ongezeko la matishio au changamoto zinazovuka mipaka ikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi, magonjwa ya mlipuko na uhalifu; umuhimu wa kulinda utu na maadili ya mtanzania; uvunaji endelevu wa rasilimali na maliasilia ikiwemo zitokanazo na uchumi wa buluu na rasilimali na maliasili zinazoendelea kugunduliwa katika ardhi na mipaka yetu; ushiriki wa makundi mengi zaidi katika jamii katika utekelezaji wa sera hususan vijana na wanawake.

***Mheshimiwa Rais,***

Mchakato wa mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 na maandalizi ya Toleo la mwaka 2024 la Sera hii utakayoizindua hii leo ulihusisha michango ya wadau wengi lengo likiwa kupata maoni yanayowakilisha sehemu kubwa ya wananchi wetu, waliomo ndani na nje ya Tanzania. Nikushukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa maelekezo na miongozo yako ya mara kwa mara kwa Wizara yetu ambayo imetusaidia kukamilisha jukumu hili muhimu kwa umahiri mkubwa. Aidha, nilishukuru Baraza la Mawaziri na Sekretarieti ya Baraza hilo kwa ushauri wao muhimu kwa Wizara na kwako, Mheshimiwa Rais, ambao hatimaye umetuwezesha kufanikisha dhamira ya kufanya maboresho ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001. Vivyo hivyo, natoa shukrani zangu kwa wataalamu kutoka taasisi za umma na binafsi, wananchi, wabia wa maendeleo, wanahabari, na wengine ambao kutokana na muda sitaweza kuwataja mmoja mmoja. Tunathamini sana mchango huo. **Asanteni sana**.

***Mheshimiwa Rais,***

Naomba nigusie kuwa kama nilivyotamka hapo awali, umekuwa ukitoa maelekezo ya mara kwa mara kwetu sisi Wizara. Maelekezo hayo uliyatoa katika muktadha wa vikao vya Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi vilivyofanyika Zanzibar na Kibaha, mwezi Novemba 2022 na Aprili 2024, mtawalia. Aidha, maelekezo uliyoyatoa wakati ukipokea taarifa ya Kamati Maalumu

uliyoiunda miaka miwili iliyopita chini ya Uenyekiti wa Balozi Mstaafu Yahya Simba mwezi Oktoba 2023, Ikulu, Dar es Salaam. Naomba nitoe tathmini fupi ya utekelezaji wa maelekezo hayo na kuonesha namna yalivyochangia katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara na taasisi zilizo chini yake, kama ifuatavyo:

Maelekezo uliyotoa yamegawanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo masuala ya kuzingatia katika mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001; muundo na hadhi ya Wizara; diplomasia ya uchumi; ushirikishwaji wa diaspora; kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika medani za kimataifa; na maboresho ya taasisi zilizo chini ya Wizara.

Kuhusu maelekezo ya Wizara kuhuisha muundo wake ili kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Mheshimiwa Rais tunaendelea kukushukuru kwa uamuzi wako wa kuongeza nafasi ya Naibu Waziri na Katibu Mkuu wanaoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Hatua hii imesaidia kuongeza msukumo katika kusimamia na kuratibu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, nikushukuru kwa kuridhia mapendekezo ya kuongeza kitengo kipya cha Uchambuzi wa Mikakati na Siasa za Kimataifa na kupandisha hadhi Kitengo cha Huduma za Sheria kuwa Idara kamili. Napenda kukuhakikishia kuwa, tayari mabadiliko hayo yamekamilika. Sambamba na hilo, Wizara ilifanya marekebisho ya muundo na majukumu ya Idara ya Diplomasia ya Uchumi pamoja na Ofisi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika

Mashariki – Zanzibar ili kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na ushiriki wa Zanzibar katika masuala ya mtangamano wa kikanda.

Katika eneo lingine ulielekeza Wizara kuimarisha ushirikiano kati yake na wadau kutoka sekta ya umma na binafsi katika kuibua fursa za kiuchumi na mikakati ya kuzitumia ipasavyo. Katika kutekeleza maelekezo haya, Wizara inaendela na juhudi za kuimarisha Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na kuweka mwomgozo mzuri wa kusimamia uratibu baina ya Wizara na wadau wa ndani na nje ya serikali.

Hali kadhalika, ulielekeza Balozi kuongezewa fedha na vitendea kazi ili kutekeleza kikamilifu majukumu, kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa majengo chakavu, kujenga majengo mapya na vitega uchumi Balozini. Wizara imeendelea kushirikiana na wadau Wengine hususan Wizara ya Fedha kuimarisha upatikanaji wa rasilimali na vitendea kazi. Wizara itaendela kuchukua hatua zaidi kuimarisha utendaji kazi katika eneo hili.

Kuhusu utambuzi wa diaspora ili kuongeza mchango wao katika maendeleo ya taifa, napenda kukujulisha kuwa, Wizara imekamilisha maandalizi ya usajili wa diaspora kidijitali (Diaspora Digital Hub) utakaoisaidia Serikali kuwa na kanzidata ya diaspora inayoonesha wasifu wao kwa maana ya mahali walipo na ujuzi walio nao.

Katika eneo la mkakati wa namna ya kutumia fursa za ongezeko la mahitaji ya matumizi ya Kiswahili kimataifa, naomba nikujulishe kuwa, wizara imechukua hatua katika eneo hili ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumzi ya Kiswahili katika vyombo vya kikanda na Kimataifa. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza programu za mafunzo ya lugha ya Kiswahili na kuanzisha ushirikiano wa kimkakati na mamlaka au taasisi binafsi kwa ajili ya kuongeza matumizi ya Kiswahili katika maeneo ya uwakilishi.

Kuhusu kusimamia maboresho ya kiutendaji katika taasisi zilizo chini ya Wizara naomba nikujulishe kuwa, tayari Wizara imefanya mapitio ya utendaji kazi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, chini ya uenyekiti wa Balozi Mstaafu Khamisi Kagasheki. Matokeo ya Tathmini hiyo yanasadia katika mageuzi na maboresho ya Kituo ili kuakisi maono yako na kukifanya Kituo kiendane na hadhi ya Mwanadiplomasia Nguli Balozi Dkt. Salim Ahmed Salim na kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Aidha, Wizara inaendelea na kufanya maboresho makubwa ya kiutendaji katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha, ambayo yamesaidia Kituo hicho kuendelea kujiendesha kwa faida. Nitumie fursa hii kukushukuru kwa kutupatia Kibali cha ujezi wa Kituo kipya cha Mount Kilimanjaro International Convention Centre kichotarajiwa kujengwa jijini Arusha kwa ubia na PSSSF.

***Mheshimiwa Rais,***

Leo, mimi siyo mzungumzaji mkuu katika hafla hii. Jukumu nililopewa ni la kukukaribisha Mheshimiwa Rais, uzungumze na hadhira iliyo mbele yako. Tuna shauku kubwa na tupo tayari kusikia nasaha zako na kupokea miongozo, maelekezo na maono yako juu ya mwelekeo wa Taifa letu, hususan katika medani za kimataifa. Lakini kabla sijakukaribisha Mheshimiwa Rais uzungumze na hadhira hii, naomba uniruhusu nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza ka Mapinduzi azungumze nasi.

Mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba sasa ni wakati wa kazi. Nitoe rai kwetu sote kutafsiri kaulimbiu ya Serikali isemayo "Kazi Iendelee", katika kutekeleza Sera hii kwa vitendo na mafanikio. Kila mmoja wetu arudi kwenye eneo lake la wajibu akiwa na shauku mpya na mpango mkakati wa kutekeleza Sera hii. Naamini kwa moyo wote kwamba tukidhamiria, tutashuhudia Tanzania mpya katika mahusiano ya kimataifa , Tanzania yenye sauti ya kusikika na yenye uwezo wa kuleta manufaa kwa wananchi wake kutokana na fursa za ushirikiano na jumuiya ya kimataifa.

Ni imani yangu kubwa kuwa, taswira ya Tanzania kimataifa itaimarika zaidi na kuwa ya nchi inayopiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali. Tumelenga kuendeleza heshima tuliyoachiwa na waasisi wa taifa letu ya kuwa taifa la wastaarabu, linalopenda amani, utu na usawa na wakati huo huo tukiiongezea sura ya ubunifu, uchapakazi na ushindani wa kiuchumi.

Kwa haya machache, naomba kwa heshima na taadhima kukukaribisha Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili uzungumze na hadhira hii.

**Karibu sana Mheshimiwa Rais.**

**Asanteni kwa kunisikiliza!!!**